JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

# BAJETI YA SERIKALI YA MWAKA WA FEDHA 2022/23 KWA LUGHA RAHISI

## Toleo la Mwananchi

IMETOLEWA NA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA KUSHIRIKIANA NA POLICY FORUM

Idara ya Usimamiz wa Bajeti ya Serikali
Wizara ya Fedha na Mipango,
Mtaa wa Hazina, S. L. P 2802, Dodoma.

## YALIYOMO


*Ukurasa wa 1,*
- **Utangulizi**
  *Bajeti ya Serikali ni nini ?*

*Ukurasa wa 2,*
- **Vipaumbele vya Bajeti**

*Ukurasa wa 3,*
*Sera na Mikakati ya Kuongeza Mapato Mwaka 2022/23*

*Ukurasa wa 4,*
*Mkakati wa kubana Matumizi Mwaka 2022/23*
- **Mapato na Matumizi**

*Ukurasa wa 5,*
*Mgawanyo wa Matumizi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa*

*Ukurasa wa 6,*
- **Mgawanyo wa Bajeti Kisekta**
  *Seka ya Elimu, Seka ya Afya*

*Ukurasa wa 7,*
*Huduma za Utawala na Deni la Serikali*

*Ukurasa wa 8,*
*Ulinzi, Usalama na Utii wa Sheria*
*Sekta ya Maendeleo ya Uchumi, Sekta ya Kilimo, Madini*

*Ukurasa wa 9,*
*Nishati, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano*

*Ukurasa wa 10,*
*Maliasili, Utalii na Mazingira, Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Kazi, Maendeleo ya Vijana na Kukuza Ujuzi*

*Ukurasa wa 11,*
*Sekta ya Hifadhi ya Jamii, Maji, Makazi na Maendeleo ya Jamii, Maji, Ardhi, Nyumba na Makazi*

*Ukurasa wa 12,*
*Maendeleo ya JamiiBiashara, Kazi, Utamaduni, Sanaa na Michezo*
- **Maboresho ya Mifumo ya Kodi, Ada na Tozo**
  *Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), SURA 148*

*Ukurasa wa 13,*
*Sheria ya Kodi ya Mapato SURA 332*

*Ukurasa wa 14,*
*Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147, Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004*

*Ukurasa wa 15,*
*Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290, Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Sura 263, Sheria ya Madini, SURA 123, Sheria ya Korosho, SURA 203, Sheria ya Bima, SURA 394.*

*Ukurasa wa 16,*
*Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, SURA 437, Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, SURA 306,Sheria ya Magari ya Kigeni, SURA 84*

*Ukurasa wa 17,*
- *Jedwali 1: Muhtasari wa Mgawanyo wa Bajeti Kisekta*

*Ukurasa wa 19,*
- **Nyaraka Rejea za Bajeti**

*Ukurasa wa 20,*
- *Kwa maoni yako jaza ukurasa huu na kutuma wizara ya fedha na mipango*



Raisi wa awamu ya sita wa Tanzania
**Mhe. Samia Suluhu Hassan**

## 1. UTANGULIZI

Kijitabu cha Bajeti ya Serikali Toleo la Mwananchi kinatoa muhtasari wa sera na mipango iliyomo katika bajeti ya Serikali kwa lugha rahisi. Lengo la kijitabu hichi ni kuongeza uelewa, uwazi, na uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za umma. Sera na mipango iliyomo katika bajeti ya Serikali hugusa maisha ya kila mwananchi kwa namna mbalimbali, hivyo ni muhimu mwananchi kupata uelewa na kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo iliyoainishwa.

### 1.1 Bajeti ya Serikali ni nini ?

Bajeti ya Serikali ni mpango unaobainisha namna Serikali itakavyokusanya mapato na kutumia katika mwaka husika ili kutekeleza shughuli mbalimbali kwa ajili ya ustawi wa jamii. Msingi wa bajeti ya Serikali ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 137 (1) ambayo inaeleza, "Rais atatoa maagizo kwa watu wanaohusika kwamba, watengeneze na kuwasilisha kwenye Bunge katika kila mwaka wa fedha wa Serikali,

makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kipindi cha mwaka wa fedha unaofuata".




## 2. VIPAUMBELE VYA BAJETI

Katika bajeti ya mwaka 2022/23, Serikali imeendelea kuzingatia maeneo matano (5) ya vipaumbele vya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26. Bajeti imejielekeza katika kuimarisha sekta za uzalishaji zikiwemo **kilimo, mifugo, uvuvi, nishati na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji** ili kujenga uchumi, kukabiliana na umasikini pamoja na ukosefu wa ajira hususani kwa vijana.


Nguzo za umeme Gridi ya Taifa

## 3. SERA ZA BAJETI NA UCHUMI JUMLA




### 3.1. Shabaha za Uchumi Jumla

Shabaha za Uchumi Jumla katika kipindi cha mwaka 2022/23 ni kama ifuatavyo:


i. Ukuaji wa Pato Halisi la Taifa (GDP) kufikia asilimia 4.7 mwaka 2022 na asilimia 5.3 kwa mwaka 2023;
ii. Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 hadi 7.0 katika muda wa kati;
iii. Mapato ya ndani kufikia asilimia 14.9 ya Pato la Taifa (GDP) mwaka 2022/23;
iv. Mapato ya kodi kufikia asilimia 11.7 ya Pato la Taifa (GDP) mwaka 2022/23; na
v. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

### 3.2 Sera na Mikakati ya Kuongeza Mapato Mwaka 2022/23

i. Kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kufanya makadirio ya kodi kwa wafanyabiashara wadogo ambao hawana uwezo wa kutunza kumbukumbu na kutengeneza hesabu za biashara zao;
ii. Kuwekeza kwenye matumizi ya teknolojia ili kurahisisha uwasilishaji wa ritani za kodi kielektroniki na ulipaji kodi kwa wakati;
iii. Kuimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo Serikalini - GePG na kuhimiza malipo ya Serikali kutumia Namba ya Kumbukumbu ya Malipo;

iv. Kuimarisha mifumo ya usimamizi katika mashirika, taasisi za umma na wakala za serikali ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha gawio na michango stahiki inawasilishwa kwa wakati;
v. Kuendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa kuipa nafasi zaidi sekta binafsi ili kuongeza mchango katika kukuza uchumi, kutoa ajira na kuongeza mapato; na
vi. Kuendeleza uanzishwaji wa vituo vya pamoja vya utoaji huduma ili kuwezesha huduma muhimu zinazo hitajika katika kuanzisha na kufanya biashara kupatikana sehemu moja.

## 3.3 Mkakati wa Kubana Matumizi Mwaka 2022/23






Katika mwaka 2022/23, Sera za Matumizi zitajikita katika kubana na kuondoa matumizi yasiyo ya lazima. Hatua za kutekeleza sera hizi ni za muda wa kati na muda mrefu ambazo ni:

i. Kudhibiti gharama zinazotokana na ununuzi na matumizi ya magari;
ii. Kufanya maboresho katika mfumo wa ununuzi wa umma kwa kuhakikisha bei za bidhaa na huduma zinazotumika sokoni zinaingizwa kwenye mfumo wa TANePS na kuwa kikomo cha bei zitakazotumika Serikalini;
iii. Kuendelea kutumia mifumo ya TEHAMA katika utekelezaji wa shughuli za Serikali;
iv. Kumuongezea rasilimali watu na fedha ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali ili kumwezesha kukagua thamani ya fedha na kufanya ukaguzi kwa wakati; na
v. Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa ulipaji wa mishahara ya watumishi wa umma.

# 4. MAPATO NA MATUMIZI

Katika mwaka 2022/23, Serikali imepanga kukusanya na kutumia jumla ya shilingi trilioni 41.48. Mapato yanatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo mbalimbali na kuelekezwa katika maeneo muhimu ya matumizi.




## 4.1 Mgawanyo wa Matumizi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa

Baadhi ya maeneo ya vipaumbele vya matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ni:

i. Shilingi bilioni 346.5 kwa ajili ya Elimu Bila Ada;

ii. Shilingi bilioni 257.4 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, mabweni, mabwalo, nyumba za shule, uzio wa mabweni 99 ya watoto wenye mahitaji maalum, matundu ya vyoo, shule shikizi za msingi na maabara za shule za sekondari;


iii. Shilingi bilioni 98.0 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya utawala, nyumba za wakurugenzi na wakuu wa idara;

iv. Shilingi bilioni 75.9 kwa ajili ya mikopo kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu;

v. Shilingi bilioni 40.1 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati ili kuziongezea mapato ya ndani Mamlaka za Serikali za Mitaa;

vi. Shilingi bilioni 20.3 kwa ajili ya kulipa posho za madiwani; na

vii. Shilingi bilioni 15.9 kwa ajili ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo.



# 5. MGAWANYO WA BAJETI KISEKTA

## 5.1 Sekta ya Elimu

Sekta ya Elimu imetengewa shilingi trilioni 5.7. Fedha hizi zitatumika katika maeneo ya vipaumbele kama ifuatavyo:

i. Shilingi trilioni 4.4 kwa ajili ya elimu ya awali, msingi na sekondari, vyuo vya ualimu, ukaguzi wa shule, elimu ya watu wazima na elimu isiyo rasmi;
ii. Shilingi trilioni 1.0 kwa ajili ya elimu ya juu, sayansi na teknolojia ikijumuisha shilingi bilioni 570 kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu;
iii. Shilingi bilioni 145.0 kwa ajili ya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi; na
iv Shilingi bilioni 97.9 kwa ajili ya matumizi ya utawala.

Aidha, hatua za kimkakati za kuboresha Sekta ya Elimu kwa mwaka 2022/23 ni kama ifuatavyo:

i. Kuanzisha dirisha maalumu kupitia TASAF kwa ajili ya kusaidia watoto wanaotoka katika familia maskini;
ii. Kujenga mabweni ya watoto wa kike kwenye maeneo hatarishi;
iii. Kuimarisha elimu ya ufundi hususani katika vyuo vya kati kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kujiajiri au kuajiriwa;
iv. Kuongeza wigo wa utekelezaji wa programu ya Elimu Bila Ada kwa kufuta ada kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita; na
v. Kujenga vyuo vya ufundi stadi katika Mkoa wa Songwe na wilaya 36 ambazo hazina vyuo.




## 5.2 Sekta ya Afya

Sekta hii imetengewa jumla ya shilingi trilioni 2.1. Baadhi ya maeneo ya kipaumbele ni kama ifuatavyo:

i. Shilingi bilioni 941.9 ni kwa ajili ya kuboresha huduma na miundombinu ya afya katika zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya;

ii. Shilingi bilioni 862.0 kwa ajili ya kuboresha huduma za tiba na miundombinu katika hospitali za rufaa ngazi ya kanda na taifa;

iii. Shilingi bilioni 258.4 kwa ajili ya huduma za kinga ikiwemo ununuzi na usambazaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo;

iv. Shilingi bilioni 85.8 kwa ajili ya kugharamia shughuli za utawala na rasilimali watu katika utoaji wa huduma za afya; na

v. Shilingi bilioni 1.0 kwa ajili ya kuboresha huduma ya afya na miundombinu katika hospitali za rufaa za mikoa.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Samia Suluhu Hassan,** akipata maelezo kutoka kwa Daktari wa Kitengo cha Magonjwa ya Figo katika Hospitali ya kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Mkoani Mara.*

## 5.3 Huduma za Utawala na Deni la Serikali

Serikali imetenga shilingi trilioni 16.8 kwa ajili ya Huduma za Utawala na kugharamia deni la Serikali. Mchanganuo wa matumizi ya sekta hii ni kama ifuatavyo:

i. Shilingi trilioni 9.1 kwa ajili ya ulipaji wa deni la Serikali;

ii. Shilingi trilioni 3.8 kwa ajili ya shughuli za utawala;

iii. Shilingi trilioni 3.7 kwa ajili ya shughuli za fedha na uchumi ikijumuisha shilingi bilioni 400.9 kwa ajili ya Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika tarehe 23, Agosti 2022; na

iv. Shilingi bilioni 208.0 kwa ajili ya shughuli za mambo ya nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki.



## 5.4 Ulinzi, Usalama na Utii wa Sheria

Shilingi trilioni 4.2 zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha ulinzi, usalama na usimamizi wa mifumo ya haki na utoaji haki ikiwemo ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya mahakama.

## 5.5 Sekta ya Maendeleo ya Uchumi

Sekta ya Maendeleo ya Uchumi imetengewa shilingi trilioni 9.1. Mchanganuo wa baadhi ya matumizi ya sekta hii ni kama ifuatavyo:

### 5.5.1 Sekta ya Kilimo

Sekta ya Kilimo ikijumuisha mifugo na uvuvi imetengewa shilingi trilioni 1.2 kwa ajili ya kutekeleza malengo ya kimkakati na vipaumbele vya Kitaifa kwenye sekta hii kwa mchanganuo ufuatao: -

i. Shilingi bilioni 300.0 kwa ajili ya kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika skimu mpya 25 zenye jumla ya hekta 53,234;

ii. Shilingi bilioni 268.9 kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ikiwemo shilingi bilioni 100.6 ya ruzuku ya mbolea na shilingi bilioni 3.0 kwa ajili ya kilimo cha vizimba (block farming) kwa vijana;

iii. Shilingi bilioni 135.7 kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya uvuvi ikiwemo Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish);

iv. Shilingi bilioni 50.0 kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi Kilwa; na

v. Shilingi bilioni 46.7 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Sekta ya Mifugo




### 5.5.2 Madini

Serikali imetenga shilingi bilioni 83.3 kwa ajili ya sekta ndogo ya madini ikilenga kuongeza mchango wa sekta hii kwenye ukuaji wa uchumi. Shughuli za kipaumbele ni pamoja na: kuwaendeleza wachimbaji wadogo; kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya uchenjuaji, uyeyushaji, usafishaji na utengenezaji wa bidhaa za madini; kufanya tafiti za madini; na kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

### 5.5.3 Nishati

Sekta ndogo ya Nishati imetengewa shilingi trilioni 2.9 kwa ajili ya:

i. Kugharamia miradi ya kuzalisha umeme ikiwemo Bwawa la Julius Nyerere MW 2,115, Maporomoko ya Maji ya Rusumo MW 80, Ruhudji MW 358, na Rumakali MW 80;
ii. Kusambaza umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA);
iii. Ujenzi wa njia za kusafirisha umeme kutoka Rufiji – Chalinze - Kinyerezi - Dodoma na Singida – Arusha – Namanga pamoja na mradi wa kufikisha umeme katika vitongoji; na
iv. Miradi ya petroli na gesi asilia ikiwemo usambazaji wa gesi asilia viwandani, utafiti wa mafuta na gesi asilia, kuchakata na kusindika gesi asilia, na uimarishaji wa mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja.




### 5.5.4 Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

Sekta ndogo ya ujenzi na uchukuzi imetengewa shilingi trilioni 3.9 kugharamia shughuli mbalimbali ikiwemo:

i. Shilingi trilioni 1.4 kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kisasa SGR, Mfuko wa Reli na ukarabati wa reli ya TAZARA;
ii. Shilingi trilioni 1.3 kwa ajili ya miradi ya ujenzi na ukarabati wa barabara;
iii. Shilingi bilioni 488.4 kwa ajili ya kukamilisha malipo ya ununuzi wa ndege, ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege; na
iv. Shilingi bilioni 100.1 kwa ajili ya uboreshaji wa bandari ya Dar es Salaam.



*Daraja la JP Magufuli, linalojengwa jijini Mwanza litakalo ziunganisha wilaya za Misungwi na Sengerema kupitia Ziwa Victoria linatarajiwa kuwa daraja refu kuliko yote Afrika Mashariki na Kati na litakuwa la sita kwa urefu katika Bara la Afrika kwa takwimu za sasa.*



*Kipande cha Reli ya Kisasa (SGR) Ruvu Station*

### 5.5.5 Maliasili, Utalii na Mazingira

Sekta hii imetengewa shilingi bilioni 615.4 kwa ajili ya; kukuza utalii wa ndani; kutangaza utalii; kuibua masoko mapya ya utalii; kukarabati na kuimarisha miundombinu katika maeneo ya hifadhi; kuibua na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati; pamoja na usimamizi na uhifadhi wa mazingira.

### 5.5.6 Uwekezaji, Viwanda na Biashara

Serikali imetenga shilingi bilioni 282.9 kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali zikiwemo:

i. Shilingi bilioni 12.8 kwa ajili ya kuboresha mazingira ya biashara na maendeleo ya viwanda, kuongeza tija na ufanisi kwenye uzalishaji wa viwanda na ufuatiliaji wa masoko;

ii. Shilingi bilioni 10.4 kwa ajili ya uendelezaji wa bidhaa za ngozi, ujenzi wa miundombinu ya uwekezaji wa viwanda na uchakataji wa mafuta ya kula;

iii. Shilingi bilioni 3.7 kwa ajili ya kukuza masoko ya bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini na kukuza sekta binafsi; na

iv. Shilingi bilioni 2.0 kwa ajili ya utafiti, ugunduzi mafunzo ya elimu ya biashara kwa wadau na kuimarisha mifumo ya TEHAMA.

### 5.5.7 Kazi, Maendeleo ya Vijana na Kukuza Ujuzi

Sekta ndogo ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Kukuza Ujuzi imetengewa shilingi bilioni 31.2 kugharamia shughuli za vipaumbele ikiwemo:

i. Shilingi bilioni 21.2 kwa ajili ya kuwezesha shughuli za kazi na ajira ikiwa ni pamoja na kuimarisha ofisi za kazi mikoani ili kudhibiti na kusimamia vibali vya kazi na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali;

ii. Shilingi bilioni 9.0 kwa ajili ya kuwezesha Programu ya Kukuza Ujuzi na Kuongeza Fursa za Ajira na Kazi zenye Staha; na

iii. Shilingi bilioni 1.0 kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

## 5.6 Sekta ya Hifadhi ya Jamii

Sekta ya Hifadhi ya Jamii imetengewa shilingi trilioni 2.2 kwa ajili ya kugharamia utoaji wa huduma za msingi kwa wazee wasiojiweza, kutokomeza ukatili wa kijinsia na watoto walio katika mazingira hatarishi, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii; na Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF).

## 5.7 Maji, Makazi na Maendeleo ya Jamii

Sekta hii imetengewa shilingi trilioni 1.3 kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali zinazohusu maji, makazi na maendeleo ya jamii kama ifuatavyo:

### 5.7.1 Maji

Serikali imetenga shilingi bilioni 723.8 kwa ajili ya sekta ndogo ya maji ili kutekeleza shughuli mbalimbali za kipaumbele ikiwemo miradi ya kusambaza maji mijini na vijijini. Baadhi ya miradi ya kipaumbele ni pamoja na:

i. Shilingi bilioni 249.1 kwa ajili ya mradi wa kusambaza maji vijijini na usafi wa mazingira;

ii. Shilingi bilioni 181.0 kwa ajili ya mradi wa kukarabati miundombinu na kusambaza maji mijini;

iii. Shilingi bilioni 46.6 kwa ajili ya mradi wa maji safi na usafi wa mazingira katika jiji la Dar es Salaam na mkoa wa Pwani;

iv. Shilingi bilioni 29.9 kwa ajili ya mradi wa kutambua, kutunza, kusimamia na kuendeleza rasilimali maji; na

v. Shilingi bilioni 28.9 kwa ajili ya mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka Tinde hadi Shelui.



*Mhe Rais Samia Suluhu Hassan akizindua mradi wa maji Mlandizi – Chalinze - Mboga*

### 5.7.2 Ardhi, Nyumba na Makazi

Sekta hii ndogo imetengewa shilingi bilioni 118.6 kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za kipaumbele ikiwemo: uandaaji wa hati, kusajili na kutoa hatimiliki na hati za hakimiliki za kimila kwa wananchi; kuboresha miundombinu ya upimaji na ramani; kushughulikia migogoro ya ardhi; kuboresha mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu za ardhi kwa njia za kielektroniki; utambuzi, upangaji miji, upimaji na urasimishaji wa makazi kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji na sekta binafsi; na uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika ngazi za wilaya.

### 5.7.3 Maendeleo ya Jamii

Shilingi bilioni 455.2 zimetengwa kwa ajili ya sekta ndogo ya maendeleo ya jamii. Baadhi ya shughuli zitakazogharamiwa ni pamoja na kuimarisha: utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii nchini; ushiriki wa jamii katika shughuli za maendeleo, upatikanaji wa haki na maendeleo ya mtoto, uwezeshaji wa makundi maalum ikiwemo machinga.

### 5.7.4 Utamaduni, Sanaa na Michezo

Jumla ya shilingi bilioni 35.4 zimetengwa kwa ajili ya kukuza, kuendeleza Sanaa, michezo na utamaduni. Maeneo ya kipaumbele yatakayotekelezwa ni pamoja na: ujenzi na ukarabati wa viwanja, vituo vya mazoezi na kupumzikia; kugharamia Mfuko wa Sanaa na Utamaduni; kuendeleza vipaji vya michezo; na kuwezesha timu za Taifa.

## 6. MABORESHO YA MIFUMO YA KODI, ADA NA TOZO

Serikali imefanya maboresho ya mifumo ya kodi, ada na tozo kwa lengo la kuongeza kasi ya kufufua uchumi na kuimarisha sekta za uzalishaji kwa ajili ya kuboresha maisha ya watanzania, hususani katika sekta ya kilimo, mifugo, uvuvi na viwanda, na kuongeza mapato ya Serikali. Baadhi ya maeneo yaliyoboreshwa ni kama ifuatavyo:

### 6.1 Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), SURA 148

*a. Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye:*

i. Vifaa vya kupima hali ya udongo kwa ajili ya kukuza utafiti na kuendeleza sekta ya kilimo pamoja na vifaa vya kupima hali ya hewa;

ii. Vyandarua vinavyotumika katika uzalishaji wa mbogamboga na maua (agro-net) kwa ajili ya kukuza sekta ya kilimo na kuongeza tija kwenye uzalishaji;

iii. Magari yenye jokofu (refrigerated trucks) na vyumba vya ubaridi (cold rooms) kwa ajili ya kuzuia mazao kuharibika baada ya mavuno na kuchochea kilimo cha kisasa;

iv. Malighafi na mashine za kutengeneza mbolea ili kutoa unafuu kwa wazalishaji wa mbolea na kuvutia uwekezaji nchini;

v. Maziwa ya mtindi (yoghurt), maziwa yanayozalishwa kwa joto la juu na kudumu kwa muda mrefu(UHT Milk) pamoja na vifungashio vya maziwa kwa ajili ya kuwawezesha wazalishaji wa ndani kushindana kikanda na kimataifa, kuongeza ajira na kuboresha maisha ya watu;

vi. Vifaa vya kielektroniki kwa ajili ya utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo nchini, vifaa vya machinjio na mbegu za malisho ya mifugo;

vii. Nyavu za kuvulia (fishing nets), ndoano (fishing hooks), na kamba za kufungia ndoano (fishing lines) kwa lengo la kukuza wavuvi wadogo; na

viii. Mafuta ya kula yanayozalishwa nchini kwa mbegu zinazozalishwa nchini kwa kipindi cha mwaka mmoja, malighafi za uzalishaji wa mafuta ya kula na vifungashio vinavyotumika kwenye uzalishaji wa mafuta.

*b. Kuanza kukusanya kodi ya ongezeko la thamani katika biashara mtandao (digital services) kwa kurahisisha utaratibu wa usajili wa walipakodi wanaotoa huduma za kidijitali bila ya kuwa na makazi hapa nchini; na*

*c. Kufuta msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye:*

i. Simu janja za mkononi (smartphones), vishikwambi (tablets) na modemu; na

ii. Huduma za kukodi ndege (air charter services).

## 6.2 Sheria ya Kodi ya Mapato SURA 332

i. Kuweka kiwango cha asilimia 3.5 cha kodi ya mapato kwa walipakodi wenye mauzo yanayozidi shilingi milioni 11 lakini yasiyozidi shilingi milioni 100 kwa mwaka;

ii. Kuondoa msamaha wa kukata kodi ya zuio kwenye malipo ya upangishaji nyumba, vyumba na majengo ya biashara;

iii.Kusamehe kodi ya zuio kwenye kuponi za hati fungani za makampuni na manispaa; na

iv. Kutoza kodi ya mapato ya asilimia 2 kwenye malipo yanayofanywa kwa watoa huduma za kidijitali wa kigeni.

### 6.3 Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147

i. Kupunguza ada ya leseni kwa wazalishaji na waingizaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa kutoka shilingi 500,000 hadi shilingi 300,000;

ii. Kusamehe ushuru wa bidhaa kwenye vifungashio vya maua, matunda, na mbogamboga; na

iii. Kutoza ushuru wa bidhaa wa shilingi 1,000 kwa kilo ya bidhaa za sukari zinazoingizwa kutoka nje ya nchi.

### 6.4 Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004

i. Kurejesha utozaji wa ushuru wa forodha wa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mafuta ghafi ya kula ya mawese (crude palm oil);

ii. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye mafuta ghafi ya soya, karanga, nazi na haradali;

iii. Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 au dola za Marekani 500 kutoka asilimia 35 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kwa mwaka mmoja kwenye mafuta ya kula yaliyochakatwa kwa kiwango cha kati na cha mwisho (semi-refined and refined);

iv. Kuongeza ushuru wa forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye nyuzi za pamba (cotton yarn);

v. Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 0 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza viongeza ladha kwenye vyakula na vinywaji (food flavors) kwa utaratibu wa *Duty Remission*;

vi. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye sukari ya matumizi ya kawaida inayoagizwa kutoka nje ya nchi kwa vibali maalum kwa ajili ya kuziba pengo la uzalishaji hapa nchini;

vii. Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye hema za chuma (prefabricated building) zitakazoagizwa na wafugaji kwa utaratibu wa *Duty Remission*;

viii. Kuongeza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 kwenye nywele bandia; na

ix. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 35 kwenye sigara za kielektroniki.

### 6.5 Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438

Kuweka sharti kwa kila mtanzania mwenye kitambulisho cha Taifa kupata Namba ya Mlipa Kodi na kuhakikisha Namba ya Mlipakodi inayotolewa inaoanishwa na Namba ya Kitambulisho cha Taifa.

### 6.6 Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290

i.Kusamehe ushuru wa mazao kwenye mbegu (seeds); na

ii.Kupunguza ushuru wa mazao ya misitu (forest produce cess) kutoka asilimia 5 hadi asilimia 3.

### 6.7 Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Sura 263

Kupunguza kiwango cha mchango wa fidia kwa wafanyakazi kwa sekta binafsi kutoka asilimia 0.6 inayotozwa sasa hadi asilimia 0.5 ya mapato ghafi ya wafanyakazi.

### 6.8 Sheria ya Madini, SURA 123

i.Kupunguza kiwango cha mrabaha (royalty) kutoka asilimia 3 hadi 1 kwenye makaa ya mawe yanayotumika kama malighafi ya kuzalisha nishati viwandani; na

ii.Kupunguza kiwango cha kutoza mrabaha kutoka asilimia 6 hadi 4 kwa dhahabu inayouzwa kwenye vituo vya kusafishia madini (refinery centres).

### 6.9 Sheria ya Korosho, SURA 203

Kugawanya mapato yatokanayo na tozo ya kusafirisha korosho ghafi nje ya nchi kama ifuatavyo: asilimia 50 ipelekwe Wizara ya Kilimo kwa ajili ya ruzuku ya pembejeo na Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo (ADF); na asilimia 50 ipelekwe Mfuko Mkuu wa Serikali.

### 6.10 Sheria ya Bima, SURA 394

Kuongeza wigo wa bima ya lazima (mandatory insurance) kwa kujumuisha masoko ya umma, majengo ya biashara, bidhaa zote zinazoagizwa kutoka nje, vyombo vya baharini na vivuko.

### 6.11 Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, SURA 196

Kutoza tozo ya asilimia 30 au dola za Marekani 150 kwa kila tani moja ya ujazo (kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa) kwenye shaba chakavu (copper waste) na vyuma chakavu (scrap metals).

### 6.12 Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, SURA 437

Kupunguza tozo ya miamala kutoka kiwango kisichozidi shilingi 7,000 hadi kiwango kisichozidi shilingi 4,000 katika miamala ya kutuma na kutoa pesa na kuongeza wigo wa tozo hiyo ili kuhusisha miamala yote ya kielektroniki.

### 6.13 Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, SURA 306

Kuanzisha tozo kwenye malipo ya vingamuzi kwa kiwango cha kuanzia shilingi 500 na kisichozidi shilingi 2,000.

### 6.14 Sheria ya Magari ya Kigeni, SURA 84

Kupunguza tozo ya magari yenye usajili wa kigeni yanayozidi ekseli 3 kutoka dola za Marekani 16 hadi 10 kwa kila kilomita 100.

## Jedwali 1: Muhtasari wa Mgawanyo wa Bajeti Kisekta

| Sekta | Bajeti 2022/23 (bilioni) | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| **1. Elimu** | **5,684.6** | **13.70** |
| 1.1 - Elimu Msingi | 4,368.3 | 10.53 |
| 1.2 - Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi | 145.0 | 0.35 |
| 1.3 - Elimu ya Juu | 1,006.4 | 2.43 |
| 1.4 - Sayansi, Teknolojia na Ubunifu | 67.0 | 0.16 |
| 1.5 - Huduma za Utawala | 97.9 | 0.24 |
| **2. Afya** | **2,149.1** | **5.18** |
| 2.1 - Huduma za Tiba | 862.0 | 2.08 |
| 2.2 - Huduma za Kinga | 258.4 | 0.62 |
| 2.3 - Hospitali za Rufaa za Mikoa | 1.0 | 0.00 |
| 2.4 - Zahanati | 96.6 | 0.23 |
| 2.5 - Vituo vya Afya | 153.8 | 0.37 |
| 2.6 - Hospitali za Wilaya | 691.5 | 1.67 |
| 2.7 - Hospitali za Utawala | 85.8 | 0.21 |
| **3. Huduma za Utawala na Deni la Serikali** | **16,797.4** | **40.49** |
| 3.1 - Mihimili | 3,809.3 | 9.18 |
| 3.2 - Usimamizi wa Mapato na Matumizi | 3,693.1 | 8.90 |
| 3.3 - Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataif | 208.0 | 0.50 |
| 3.4 - Deni la Serikali | 9,087.0 | 21.91 |

| | | |
|---|---|---|
| **4. Ulinzi, Utawala wa Sheria na Usalama** | **4,208.0** | **10.14** |
| 4.1 - Ulinzi | 2,712.0 | 6.54 |
| 4.2 - Usalama wa Umma | 1,206.2 | 2.91 |
| 4.3 - Mahakama | 289.7 | 0.70 |
| **5. Maendeleo ya Uchumi** | **9,064.2** | **21.85** |
| 5.1 - Kilimo | 1,216.2 | 2.93 |
| 5.2 - Madini | 83.3 | 0.20 |
| 5.3 - Nishati | 2,905.9 | 7.01 |
| 5.4 - Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano | 3,929.2 | 9.47 |
| 5.5 - Maliasili, Utalii na Mazingira | 615.4 | 1.48 |
| 5.6 -Viwanda | 99.1 | 0.24 |
| 5.7- Biashara | 183.8 | 0.44 |
| 5.8 - Kazi, Maendeleo ya Vijana na Kukuza Ujuzi | 31.2 | 0.08 |
| **6. Hifadhi ya Jamii** | **2,244.2** | **5.41** |
| 6.1 - Wazee, Watoto na Watu wenye Ulemavu | 37.3 | 0.09 |
| 6.2 -Mifuko ya Hifadhi ya Jamii | 1,761.1 | 4.25 |
| 6.3 - Mfuko wa Bima ya Afya | 445.9 | 1.07 |
| **7. Maji, Nyumba na Maendeleo ya Jamii** | **1,333.1** | **3.21** |
| 7.1 - Maji | 723.8 | 1.75 |
| 7.2 - Ardhi, Nyumba na Makazi | 118.6 | 0.29 |
| 7.3 - Maendeleo ya Jamii | 455.2 | 1.10 |
| 7.4 - Habari, Michezo na Utamaduni | 35.4 | 0.09 |
| **Jumla Kuu** | **41,480.6** | **100.00** |

## NYARAKA REJEA ZA BAJETI

Ifuatayo ni orodha ya nyaraka za Serikali zilizotumika kama chanzo cha taarifa za kuandaa bajeti:

1. Dira ya Taifa ya Maendeleo, 2025;
2. Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano;
3. Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2020
4. Mfumo wa Sera za Uchumi Jumla: Unatoa taarifa juu ya sera za bajeti na maboresho;
5. Randama za Mipango ya Muda wa Kati na Mfumo wa Matumizi wa Muda wa Kati ya mwaka 2022/23;
6. Mwongozo wa Mipango na Bajeti 2022/23;
7. Hotuba za Bajeti za Wizara za Mwaka wa Fedha 2022/23;
8. Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mwaka wa fedha 2022/23;
9. Sheria ya Fedha ya Mwaka 2022;
10. Sheria ya Matumizi ya mwaka 2022;
11. Sheria ya Bajeti 2015, Sura 439;
12. Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 (Juzuu Na. I, II, III na IV);

Ili kupata baadhi ya nyaraka hizi na matoleo yaliyotangulia ya vitabu vya Bajeti ya Serikali Toleo la Mwanachi, unaweza kutembelea mitandao ya:

- Wizara ya Fedha na Mipango (www.mof.go.tz)
- Policy Forum (www.policyforum.or.tz)

Kwa maelezo zaidi kuhusu Bajeti ya Serikali Unaweza kupata taarifa zaidi kuhusu mchakato wa uandaaji wa bajeti kutoka katika vyanzo vifuatavyo:

- Nyaraka zenye taarifa za Bajeti ya Serikali (angalia orodha ya nyaraka za rejea) na hasa, nakala ngumu ya vitabu vya Bajeti ya Serikali ambavyo vinapatikana Wizara ya Fedha na Mipango S.L.P 2802, Dodoma.
- Nakala laini za vitabu vya Bajeti ya Serikali zinapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango http://www.mof.go.tz

Kumbuka kwamba ni haki yako kujua bajeti hii na taarifa nyingine zinazohusiana na Bajeti ya Serikali. Ongea na Viongozi wako kuhusu taarifa hizi na washirikishe watu wengine katika jamii unayoishi nayo.

## KWA MAONI YAKO JAZA UKURASA HUU NA KUTUMA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

Toa maoni yako kuhusu Bajeti ya Serikali ya mwaka 2022/23

---------------------------------------------------------------------------------------------------

---------------------------------------------------------------------------------------------------

---------------------------------------------------------------------------------------------------

Je, unahitaji ufafanuzi zaidi ya uliotolewa katika kijitabu hiki?

☐ NDIYO ☐ HAPANA

Kama jibu ni NDIYO Je, unahitaji ufafanuzi katika eneo gani?

---------------------------------------------------------------------------------------------------

---------------------------------------------------------------------------------------------------

---------------------------------------------------------------------------------------------------

Je, ni kwa kiasi gani kijitabu hiki kimekusaidia?

☐ Kiasi kikubwa ☐ Wastani ☐ Haki kunisaidia

Je, ni kwa kiasi gani kijitabu hiki kilikuwa rahisi kusoma na kueleweka?

☐ Rahisi ☐ Wastani ☐ Ngumu

Je, umepataje kijitabu hiki (weka alama ya V kwenye kisanduku ulichochagua)?

☐ Tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango
☐ Tovuti ya Jukwaa la Sera
☐ Taasisi za Serikali
☐ Nyingine (Tafadhali taja)

Tuma maoni yako katika anuani ifuatayo

Katibu Mkuu,
Wizara ya Fedha na Mipango,
Idara ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali, Mtaa wa Hazina,
Mji wa Serikali – Mtumba, 40468 Dodoma,
Sanduku la Barua 2802, DODOMA-TANZANIA

Au tuma kwa njia ya barua pepe kwa:
ps@mof.go.tz

*Katibu Mkuu,*
*Wizara ya Fedha na Mipango,*
*Idara ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali,*
*Mtaa wa Hazina,*
*Mji wa Serikali – Mtumba,*
*40468 Dodoma,*
*Sanduku la Barua 2802,*
*DODOMA-TANZANIA*

*ps@mof.go.tz*